

Kwa kumbukumbu ya Hamidu R. Tambwe (6 Aprili 1950 – 2 Julai 2002).

Hamidu R. Tambwe alizaliwa tarehe 06 Aprili 1950, na kufariki tarehe 02 Julai 2002. Marehemu Hamidu Tambwe ni mtoto wa marehemu Rajabu Salehe Tambwe, ambaye pia alikuwa mwandishi wa mashairi. Wakati wa uhai wake, marehemu Rajabu Salehe Tambwe alirumbana sana kishairi na Mzee Saadan Kandoro. Kwa kiasi kikubwa, ma-shairi ya Hamidu Tambwe yalikuwa zaidi maadili ndani ya familia yao, na hasa maandishi kama barua kati yake na baba yake mzazi Rajabu Salehe Tambwe.

Maandishi mengi ya kishairi ya Hamidu Rajabu yaliandikwa kati ya miaka ya 1960 na mwanzoni mwa 1970. Kazi zake kwa ujumla ni ya mashairi na tungo zaidi ya 50 hivi.

Kwa upande wa Elimu, alisomea Stashahada ya Biashara, Chuo cha Biashara cha Dar Es Salaam na Shahada ya Uchumi Chuo Kikuu cha Dar Es Salaam, (1980).